

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



### TAARIFA KWA UMMA.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leo Alhamisi , Marchi 14,2019 katika Mkutano wake wa Kawaida wa Baraza la Madiwani uliofanyika Katika Ukumbi wa Manispaa ya Kinondoni, Pamoja na Mambo mengine imethibitisha matumizi ya jumla ya **Tshs.3,675,202,443.90** zilizotumika kutekeleza Miradi ya Maendeleo robo ya pili kwa kipindi cha kuanzia mwezi oktoba hadi Desemba , 2018.

Kwa mujibu wa Mchanganuo wa Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo robo ya pili, kati ya Fedha hizo, **Tshs.2,678,384,151.30** ni fedha za mapato ya ndani ya Manispaa, **Tshs.510,438,100.00** ni fedha za mfuko wa pamoja wa Afya ,**Tshs.176,006,913.6** ni fedha za Elimu bila malipo msingi, **Tshs.176,053,020.00** ni fedha za Elimu bila malipo Sekondari, **Tshs.41,050,000.00** ni fedha za mfuko wa kuchochaea maendeleo ya Jimbo na **Tshs.93,270,259.00** ni fedha za michango ya jamii.

Aidha Baraza la Madiwani katika Mkutano huo wa Kawaida limethibitisha taarifa za utekelezaji wa kazi za Kamati za Kudumu za Halmashauri yaani Kamati ya Huduma za uchumi Afya na Elimu, Kamati ya Mipangomiji na Mazingira, Kamati ya Maadili, Kamati ya Kudhibiti Ukimwi na Kamati ya Fedha na Uongozi zilizofanyika katika robo ya Pili kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2018.

Imetolewa na:-

Sebastian Modestus Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**